# VITA 7 ZA KANISA LA MAHALA

# SMIRNA

## VITA YA DHIKI

JAMES KALEKWA

# SMIRNA:

*Vita ya dhiki*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Muktadha wa Smirna ...................................................... 4

Uelewa wa Awali ......................................................... 14

Uthibitisho wa Kimaandiko .......................................... 16

Muonekano wa Vita ya Dhiki ....................................... 19

LENGO LA VITA YA DHIKI ...................................... 23

NAMNA YA KUISHINDA VITA YA DHIKI .....**Error! Bookmark not defined.**

Kuhusu Mwandishi: ..................................................... 25

Kuhusu New Vine Church: ........................................... 25

Mawasiliano na Mwandishi: ......................................... 26

# Muktadha wa Smirna

Sminrna ulikuwa na mji wenye uzuri wa miondombinu, maua na hali ya hewa. Fahari na majivuno ya mji na watu ndani yake ilikuwa ni ukuu na uzuri wa mji mpaka mwaka 600 K.K ambapo watawala wa himaya ya Lydia walipouvamia na kuangamiza kisha kuuacha kama kijiji fukara - Mji uliokufa. Alekzanda mkuu akiwa kwenye mji huo, aliona maono kwenye ndoto ya kuufufua mji kutoka kwenye maangamizo yaliyoupata mji. Kwa matengenezo aliyoyafanya mji ulifufuka na kuwa maisha bora zaidi kuliko ulivyokuwa awali. Hii ilipelekea historia na machapisho ya mji kujaa masimulizi ya namna mji ulivyokuwa "umekufa na sasa umefufuka". Na hapo ndipo alaipoanzia Bwana Yesu ili waamini waliomo mjini wamwelewe, *"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna Andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa mwisho,* ***aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai."*** Ufunuo wa Yohana 2:8

Ni mji pekee uliokuwa unafahamika kwa moja ya marashi muhimu, marhamu nzuri. Na hii ndiyo asili ya jina la mji Smirna. Ni katika msingi huu wa mji uliofufuka kiasi cha kuwa mji pekee wenye marashi na harufu nzuri – marhamu; Yesu anajitambulisha!

Moja ya viongozi waandamizi wa kanisa la Smirna, askofu Polycarp ambaye insadikiwa ya kwamba alikuwa ni mwanafunzi wa moja kwa moja wa Mtume Yohana.

Si yeye tu bali ni pamoja na Polycrates ambaye alikuwa askofu wa kanis ala Efeso baadaye. Mwaka 155 B.K Polycarp, askofu wa kanisa la Smirna ambayo kwa sasa ni mji wa Izmir, Uturuki aliuwawa kwa kuchomwa moto na kupigwa mkuki wa ubavuni.

Siku tatu kabla ya kukamatwa na kuuwawa kwake, akiwa kwenye maombi, aliona maono ya mto wa kulalia "pillow" akiwa ameulalia na umeshika moto – unawaka. Aliwaambia waliokuwa pamoja naye ya kwamba, *"Nitauwawa kwa kuchomwa moto hali nikiwa mzima."*

Maaskari shupavu na vijana wa jeshi katili la Kirumi, walitumwa na mamlaka za mji kwenda kumkamata mzee huyu, Askofu Polycarp. Walivyofika kwenye malango ya nyumba yake, aliteremka kutoka ghorfani alikokuwa amejipumzisha na kuwakaribisha. Askari walijitambulisha na kueleza nia yao ya kumkata ili akauawe. Hata hivyo, askofu alikuwa na maombi mawili; kwanza, wageni wake (maaskari) waandaliwe chakula kabla ya kutekeleza majukumu yao; pili apatiwe lau saa moja ili akafanye maombi binafsi. Akiwa kwenye maombi ndani ya ile saa moja, kulikuwa na mtembeo wa nguvu za Mungu kiasi cha wale askari kusikia mioyo yao kuhukumiwa na kuchomwa dhamiri zao. *"Kwanini tumtendee ubaya huu mtu mwema namna hii?",* askofu Polycarp aliendelea kuomba kwa saa moja zaidi. sHata hivyo, askari walikuwa watiifu kwa kiapo cha kazi na majukumu yao – walimkamta.

Alipofikishwa mahala pa mateso, kwa sababu ya umri mkubwa, yule mtesaji aliingiwa na huruma. Badala ya kumtesa, alimshauri amkane Yesu ili abaki kuwa salama. Ndipo askofu Polycarp alinena usemi ule maarufu kwenye ulimwengu wa ukristo, *"Miaka 86 nimemtumikia, hajanitenda uovu wowote. Ni jinsi gani ninaweza kumkana mfalme na mwokozi wangu?"*. Yule mtesaji aliudhiwa na ujasiri wa mzee Polycarp, kwa hasira alimtishia ya kwamba ataachilia wanyama wakali wamrarue na kuyahitimisha maisha yake; askofu Polycarp hakutetereka. Kisha yule mtesaji alimwambia kuhusu moto mkali ulioandaliwa mbele yake iwapo hatamkana Yesu. Askofu alimjibu, *"Unanitisha kwa moto ambao unaweza kuunguza kwa saa, kisha ukazimika. Laiti ungejua kuhusu moto wa milele ulioandaliwa kwa ajili ya wasiomcha Mungu… kwa nini unangoja? Leta chochote ulichondaa kwa ajili ya mauti yangu."*.

Baada ya majibizano hayo kutokuwa na faida yoyote. Mtesaji aliamuru askofu Polycarp auwawe kwa kuchomwa moto. Ilivyo desturi, watu hugongomelewa mtini ili wanapochomwa moto wasikimbie. Askofu alisisitiza ya kwamba hakuna haja ya kufanya hivyo, bali wamfunge tu mikono yake kwa kamba. Aliingizwa kwenye moto wenye kuni nyingi hata hivyo baada ya muda mrefu sana, hakuwa amekufa. Ule moto uligeuka na kuwa kama safina kwake. Agizo lilitolewa auawe kwa kuchomwa mkuki. Jumamosi ya Februari 23, 155

B.K, askofu Polycarp, moja ya wafia-imani kwenye ukristo aliondoka duniani.

*"... uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima."* Ufunuo wa Yohana 2:10b

# Kanisa la Smirna

*"**Naijua dhiki yako** na umaskini wako, (lakini u tajiri) najua na matukano ya hao wasemao kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani."* **Ufunuo wa Yohana 2:9**

Dhiki: Kama kuna mambo hungependa Yesu akuambie ni kuunganishwa ni dhiki kwenye utambulisho wako. Fikiria Yesu aseme *"dhiki yako"*, au *"magonjwa yako"*, au *"taabu yako"*. Ni kweli mwanadamu aliyekata tamaa anaweza kujiambatanisha na mambo ya namna hiyo, kujitaja yeye pamoja na dhiki kwenye kundi moja. Lakini moyo wake ukiinuka, hukung'uka dhiki pembeni. Kwa Smirna, swala lao ni tofauti. Ni Yesu mwenyewe ndiye anayewaambia hivyo! Uwe na uhakika Yesu hajakata tamaa au hajachoka bali anawaambie iliyo kweli. Hata hivyo ninachopenda zaidi ni kugundua ni lile neno la kwanza kwenye hiyo sentensi *"Naijua"*. Huo ni uthibitisho tena ya kwamba kila kitu kiko kwenye mikono salama. Yesu hashitukizwi na mambo (never caught by surprise). Na kama anaijua, basi anajua na hitimisho lake litakuwaje. Kanisa la Smirna na watu ndani yake wanaweza kutulia na kupumzika kwenye kweli hiyo ya kwamba "Yesu yu ajua!"

Kwani, wewe ungependa uhakikisho gani zaidi ya huu aliousema Yesu ya kwamba anajua?

Kwenye zama na nyakati za uandishi wa kitabu hiki neno dhiki lilikuwa na maana nzito na ya kueleweka kwao. Mkosaji yeyote mathalani wa matendo ya uhalifu hupewa adhabu ya dhiki. Namna ambavyo dhiki hii hutolewa nikwa kumlaza chini mhalifu, akiwa amelala chali (uso wake umetazama juu na mgongo wake ukiwa ardhini), amenyooka. Ndipo watesaji huanza kumuwekea vitu vizito kama vile mawe kifuni mwake. Baada ya muda huongeza kitu kingine kizito kifuani; na hatimaye huongeza kingine kiasi cha muhalifu kufa mwenyewe kwa kukosa nguvu ya kustahimiliki dhiki hiyo. Mara nyingi, wahalifu hawakuweza kustahimili zaidi ya awamu tatu za vitu vizito vifuani mwao.

Na hicho ndicho kilikuwa kinalitokea kanisa la Smirna – dhiki! Vitu vizito kifuani ili kulitesa kanisa life jenyewe kwa kukosa nguvu ya kustahimili. Hebu tazama ilivyo ajabu, Yesu anataja vitu vizito vitatu vinavyowekwa kwa kanisa hili.

a) **Umasikini:**

Kwenye zama hizi kuwa mkristo halikuwa jambo la kifasheni au jambo la kukubalika miongoni mwa wanajamii. Ilikuwa ni kama kuchagua kujitenga na watu wengine. Kuokoka kulimpelekea mtu asiwe sehemu ya mifumo ya kuuzalishaji mali ya wakati huo. Kulikuwa

na vyama vya ushirika ambamo wakulima na wafanyabiashara walikuwa wanachama. Hata hivyo, vyama hivi havikuishia kwenye maswala ya uchumi tu, bali viliambatanisha uchumi wao na maswala ya ibada. Vikao vya vyama hivi vya ushirika vilifanyikia kwenye mahekalu ya miungu "Athena" ambamo uovu na uchafu wa kila namna ulifanyika huko. Kukataa kuwa sehemu ya ibada za namna hiyo ni kujifuta uachama kwenye vyama vya ushirika. Hii ilipelekea hali ya umasikini wa kifedha miongoni mwa waamini na kanisa.

Hata hivyo, Bwana Yesu mwenyewe hauoni huo kuwa ni umasikini kwelikweli. Ndiyo maana anawakumbusha "lakini u tajiri". Iwapo dunia itakuminya kiuchumi ili umkane Yesu kimkakati lakini ukakaza kumpenda Yesu – wewe ni tajiri! Na hapa ninakumbuka wimbo wa kale wa maamuzi ya kumfuata Yesu uitwao "nimekubali kumfuata Yesu":

*"Nimekubali kumfuata Yesu,*
*Nimekubali kumfuata Yesu,*
*Nimekubali kumfuata Yesu*
*Sitarudiiii, Sitarudiiiii*

*Chukua vyote niachie Yesu*
*Chukue vyote niachie Yesu*
*Chukua vyote niachie Yesu*
*Sitarudiiii, Sitarudiiii"*

Sidhani kama kanisa la Smirna lilikuwa linaufahamu wimbo huu au kama ulikuwa umetungwa tayari. Lakini moyoni mwangu ninawasikia wakiimba kwa auti kuu za ushindi!

b) **Matukano:**

Unajua ukristo umetokea kwenye dini ya Uyahudi (Judaism)? Mara ya kwanza ulionekana ni kama kikundi (sect) ndani ya dini kubwa ya Uyahudi. Walitumia kitabu kimoja, waliwarejea manabii walewale, walimtaja Mungu yuleyule – Yehova, walishiriki sikukuu nyingi kwa kufanana…. Na waliabudu siku moja kwenye jengo moja liitwalo SINAGOGI! Wayahudi walipata kibali na upendeleo kutoka kwa watawala, dola ya Rumi. Hivyo hawakutaka kuharibu mahusiano yao na watawala kwa sababu kwa kufanya hivyo wangejiingiza matatani na kujivutia mateso. Ili kujinasua kutoka kwenye hali ya kufananishwa na wakristo, watu wa dini ya kiyahudi waliamua kujipendekeza kwa watawala kwa kuwasema vibaya wakristo na ibada zao.

Walianza kuishambulia ibada ya meza ya Bwana. Waliwashitaki wakristo kwa watawala ya kwamba kila wakutanapo hula mwili na damu ya Yesu. Kwa hiyo ni dini ya watu wanaokula nyama na kunywa damu – ni dini ya wauaji! Pili, waliwashitaki ya kwamba ni watu wanaoitana “kaka na dada” au kw alugha ya zama hizi “wapendwa”. Sasa kwa kuwa wao (wakristo) walikuwa

ni ndugu, maana yake walionekana na kutafsiriwa kutojali ndugu zao wengine na familia zao. Kwenye utamaduni wa Rumi (Kimsingi hata sasa kwenye nchi ya Italia na Hispania) familia ni kitu kinachokumbatiwa kwa thamani sana kuliko kitu kingine chochote. Yeyote anayekuja kuvuruga mpangilio huu wa kijamii huchukuliwa kama adui.

Hayo ndiyo matukano au dhihaka kutoka kwa watu wa dini ya Kiyahudi. Huo ni uzito wa pili uliowekwa kwenye kifua cha kanisa ili lijifie jenyewe kwa kutokustahimili.

Hata hivyo, Bwana Yesu mwenyewe anahitimisha kwa kuwaita hao kuwa ni sinagogi la shetani.

*"Naijua dhiki yako na umaskini wako, (lakini u tajiri)* ***najua na matukano ya hao wasemao kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani.****"* Ufunuo wa Yohana 2:9

Hudhani sentensi hii ya Bwana Yesu ingekutia moyo sana wakati ukikutana na matukano haya? Kumbe tunashughulika na shetani hata si Wayahudi wenyewe kimsingi.

c) Kutupwa gerezani na kuuwawa:

Uzito wa tatu unaowekwa kwenye kifua cha kanisa la Smirna ni unabii wa kile ambacho kitatokea muda si mrefu, siku za usoni ni baadhi ya waamini kwenye

kanisa hili kuburuzwa na kutupwa gerezani. Na hapa si magereza ya maalum ya kiafisa… ni eneo chafu lisilofaa mwanadamu kuishi. Na zaidi baadhi yao wangeuawa! Ndivyo ilivyotokea. Unakumbuka kisa cha Askofu wa karne ya pili wa kanisa la Smirna, askofu Polycarp?

Huo ndiyo uzito namba tatu uliowekwa juu ya kifua cha kanisa ili wafe na/au wamuache Kristo.

# Uelewa wa Awali

*"**Naijua dhiki yako na umaskini wako, (lakini u tajiri)** najua na matukano ya hao wasemao kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani."* **Ufunuo wa Yohana 2:9**

Hii ni vita ambayo inainuka kinyume chako kwa sababu wewe ni mwamini (imani uliyonayo ndani ya Kristo); Na Imani hiyo ndani ya Kristo inavyotandaa na kuathiri maeneo mengine ya kimaisha. Kwa hiyo vita hii si tu kwamba inashambulia ukristo wako bali pia na jinsi ukristo wako unavyohusika kwenye maeneo mengine ya kimaisha. Hapa ninamaanisha ni kwa namna gani imani yako ndani ya Kristo imeamua mwenendo wako wa maisha kwenye eneo la ndoa, familia, uchumi, fedha, elimu, afya, namna ya kuhusiana na watu, tabia na mwenendo na maeneo mbalimbali ya maisha.

Kazi ya vita hii ni kuzuilia maisha mwamini yasipokee hatua na uelekeo wa kiungu kwa kuwa mambo yote ya mwamini yanaendeshwa na imani yake ndani ya Kristo. Imani ikiathiriwa, maisha yameathiriwa.

Mambo yako yote ya kimaisha kama vile kibiashara, uzalishaji, ndoa, elimu, na uchumi yatakumbwa na vita hii ya dhiki kwakua umeamua kutofuata namna ya ulimwengu. Umeamua ya kwamba imani yako ndani ya

Kristo itakuwa ndiye mwamuzi wa mwisho wa namna ya kuenenda kwenye nyanja zingine zote za kimaisha.

Ushahidi mwingi wa neno la Mungu unatuonyesha uwepo na uhalisia wa vita hii; uwe unapenda au haupendi; unajua au haujui; hii vita itakuja lakini haitokaa muda wote. Ni kama vile jua ambavyo haliwaki muda wote.

# Uthibitisho wa Kimaandiko

Kwenye sura hii nimekusudia kukuonyesha kwa ushahidi wa kimaandiko ni kwa namna gani hii ni moja ya vita unapaswa kuzitarajia kwenye maisha yako ya ukristo. Ni nyenzo "muhimu" sana mikononi mwa adui kufifisha Imani ya wengi na huenda kuwaondosha hata kwenye Imani ndani ya Kristo baadhi ya waamini.

Ninapokuonyesha vita hii, simaanishi kuikuza bali kukujenga uelewa; hata hivyo imani si kukataa uwepo wa vita hii au kudharau uhalisia wake. Bali ni kuitambua na kujua namna ya kuiendea.

*"Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki maana ufalme wa Mbinguni ni wao, heri ninyi watakapo washutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo kwa ajili yangu"* **Mathayo 5:10-11**

Unaona msingi wa kuudhiwa? Ni kwa ajili ya haki! Kwa hiyo kwa kila mwenye haki wa Bwana kutakuwa na wakati fulani maishani ataudhiwa tu. Kutakuwa na nyakati za kushutumiwa, kunenewa kila aina ya neno baya kwa uongo… kwa ajili ya BWANA! Kimsingi, si maneno ya kweli. Lakini yataelekezwa kinyume chako.

*"21. Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watwaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu. 22. Lakini haya yote watawatendea*

*kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyenipeleka."* **Yohana 15:20-21**

*"Heri ninyi watu watakapowachukia, na kuwatenga, na kuwashutumu, na kulitupa nje jina lenu kama neno ovu, kwa ajili ya mwana wa Adamu."* **Luka 6:22**

Kwa maandiko hayo yaliyonukuliwa juu utaelewa huo mtiririko. Ni kwamba, mashutumu au maneno mabaya yoyote kinyume chako hayana uhalali wowote lakini bado yanaelekezwa kwako. Na sababu ya msingi ambayo tunaona inajirudirudia kwenye maandiko ni kwa sababu ya BWANA! Ndiyo kusema, ukitaka vita hii isikuelekee – muache BWANA! Huo ndiyo mwisho wa vita hii.
Lakini gharama ya kumwacha BWANA ni kubwa sana kuliko ile ya kuikabilia vita hii. Usimwache BWANA!

*"Lakini mimi nawaambia, Wependeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."* **Mathayo 5:44**

Hata kama unapenda amani kaisi gani; kaa ukijua kwa sababu uko ndani ya Kristo una maadui zako tu. Hata kama hawajawahi kujitambulisha, tunza hii kichwani. Na kuna kundi la watu ambao *"wamepakwa mafuta"* kuja kukuudhi kwenye maisha yako. Hao ndiyo mawakala wa vita ya dhiki kwenye utekelezaji wao; wengine wanajitambua na wengine hawajitambui. Wengine

wanafanya kwa kukusudia na kwa kujua; na wengine wanatumika tu kama vikaragosi.

*"29. Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, wau mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya Injili, 30. Ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele."* **Marko 10:29-30**

*"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?"* **Warumi 8:35-36**

Umeaona ya kwamba kuna hali na watu ambao wako tayari kutuweka kwenye hali ya kudhikika? Na mwisho wake ni kutufikisha mahali pa ***kutengwa na upendo wa Kristo.*** Hata hivyo hupaswi kusahau vita hii imeambatanishwa na uheri… Heri ninyi!

Nimetamani sana uone hii ni vita inayoelekezwa kwa kila mwamini ili kumtenganisha na Kristo. Kwa kuwa mwamini atachagua kubaki kwa Kristo, vita hii itajaribu mara kwa mara kumuondoa. Waamini wanaoshinda si wale wasio na dhiki bali ni wale walioweka kusudio ndani ya mioyo yao ya kwamba, *"38. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, 39. Wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe*

*kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."* Warumi 8:38-39

# Muonekano wa Vita ya Dhiki

Vita hii hujifunua na kujiwasilisha mbele ya mwamini katika sura na mwonekano wa namna mbili: Mosi, mwonekano wa maneno, na pili, mwonekano wa kuzongwa kimwili.

1. Mwonekano wa maneno

Ngazi hii inaambatana na vitu kama:

a) Uzushi ambayo ni maneno yasiyo ya kweli; hii ni njia anayoitumia adui ili ukate tamaa usiweze kuendelea katika imani ndani ya Kristo na usiweze kufikia kiwango cha matokeo ambacho Mungu amekikusudia ukifikie ukiwa hapa duniani; Uzushi hukusababisha upunguze kasi ya kufukuzia milki zako. Ni namna ambayo adui anapigana ili akuwahi usiweze kustawi na kuwa mtu mkubwa; Ieleweke ya kwamba kwa kadri unavyozidi kwenda juu unazidi kujiweka wazi kuzushiwa. Unakuwa kivutio cha uzushi!
Angalizo muhimu ni kwamba unapojiandaa kua mtu mkuu pia ujiandae kwa vita ya kuzushiwa lakini haupaswi kukata tamaa.

b) Shutuma: Haya ni maneno ya mashitaka yanayosemwa kinyume na mwamini lakini hayapelekwi kwenye maeneo au vyombo rasmi ili kuamua mashitaka hayo. Mashutumu huibuliwa na kuachwa hewani ili jamii iamue yenyewe. Utashutumiwa na watu wanakushtaki dhidi ya jamii na ndio mashtaka magumu kuliko ya mahakamani kwakua hakuna wa kukutetea. Ni vyema ukajua ya kwamba iwapo watu wakitaka kukuzushia watatafuta kitu ambacho kitawapa sababu, na haya yote ni kwa sababu wewe ni mwamini. Mara nyingi hawa watu wanaokushutumu wanakua hawakujui ni vile tu roho mchafu amewaingia. Kama huwezi kuyabeba na kushughulika na mashutumu basi simulizi yako itakuwa imeishia hapo. Hizi vita ndiyo zitaamua uwe mkuu au urudi kulala!

c) Hukumu: Hizi ni kesi za kisheria zinazopelekwa kwenye mamlaka, maeneno na vyombo rasmi vya kisheria. Hata hivyo, kesi hizi ni za kutengeneza na kubuniwa tu.

d) Matukano: Watu wataanza kukusema maneno mabaya, lugha chafu na za utusi; watakutukanisha, watatengeneza vitu vingi vya hovyo na uongo pia watatengeneza uthibitisho. Matukano yanaletwa au yanatengenezwa na watu wa karibu zaidi yako

wakati mwingine wananunuliwa ili waseme uongo. Matukano yanatokea kwa watu wa karibu sana kiasi ni ngumu kutokuamini. Matukano yanayoelekezwa kinyume chako yanaleta aibu kwa familia na watu wa karibu.

e) Ushahidi wa uongo: ushahidi unatengenezwa, kwa kadri unavyoenda juu hakikisha unakua msafi uwezekanavyo.

f) Kukukabili moja kwa moja kwa maneno: Hapa maadui na waletao dhiki hujitokeza na kukukabili. Wengine hukusema machoni pako na wengine hulitaja jina lako kwenye majukwaa (kama vile mitandao ya kijamii) na kulidhalilisha.

g) Usaliti: Mtu wa ndani anageuza maneno na ni hatari sana kwasababu kuna muda kwenye maisha mtu mmoja kati ya watu wako wa karibu atajaribiwa kukusaliti mfano mzuri ni Yuda Iskariote kwa Bwana Yesu

2. Mwonekano wa kuzongwa kimwili

Hii iko tofauti na ngazi ya maneno maana hii ni ya kufatwa hadharani, ana kwa ana, kukukabili na kukugusa kimwili kabisa. Kuna watu watakuja moja kwa moja kukuvamia wewe au mali zako na lengo lao ni upate madhara.

Katika vita hii sio busara kuanza kuchukulia mambo kibinafsi

a) Kuburuzwa kwenye mamlaka za kidunia. Haya yote yanatokea kwa sababu ni muamini wala sio uzembe au kuna vitu haujafanya vizuri. Wapo watu waliochomwa moto kwa sababu ya imani Kubali kwamba kwakua ni kazi ya Bwana kuwa tayari kuiendea. Milki haziko kwa ajiri ya waoga au watu wanaokimbia dhiki bali watu ambao hata dunia nzima ikiwa kinyume na wewe bado uendelee kusimama. Ambae anaanzisha hii vita ni ibilisi, adui ni ibilisi anatumia watu wako wa karinu na ili ushinde hii vita hautakiwi kupigana au kukasirikia watu pigana na ibilisi ndie adui sahihi.

# Lengo la Vita ya Dhiki

I. Umkane na kumuacha Yesu; maana ukimkana na kumuacha utapoteza milki yako ya milele. Hakikisha kwa chochote kitakacho kutokea haumuachi Bwana Yesu endelea kusimama; ndipo utakua umejihakikishia umilki wako wa milele.

II. Ili uwe mtu wa wastani na usiwaze mambo makubwa zaidi ubaki kuwa mtu wa kawaida.

III. Usipite njia ya Mungu kuelekea milki zako hapa duniani, shetani anatabia ya kukuhamisha uwanja ili usiweze tambua uwezo ulio nao.

# Namna ya Kuishinda Vita ya Dhiki

1. Usiogope! Yesu anatufundisha tusiogope maana adui anawashinda wengi kwa kuwapandikiza hofu.

2. Uwe mwaminifu hata kufa! Yesu anatufundisha kua ukiwa tayari hata kufa hapo ndio utaishi. Kama hauko tayari kufa hauko tayari kuishi, na kwakuwa uko tayari kufa Yesu atahakikisha unaishi. Maisha ya wastani yapo kwa watu ambao hawako tayari kufa, ukiwa tayari kulipia mauti hiyo vita utashinda.

3. Uwe tayari kulipia gharama. Maisha ya ukristo yana gharama ambayo unapaswa kuililipikia kila siku. Inaweza kuwa ni kujikana mwenyewe, kujitwika msalaba wako, au inaweza kuwa ni kuzichukua mwilini mwako chapa za Yesu Kristo, au yaweza kuwa ni kuutoa mwili wako kila siku kuwa dhabihu iliyohai ya kumpendeza… kuna gharama ya kulipia! Baba yangu, pastor Goodluck Kayara amewahi kunifundisha ya kwamba tofauti ya wanaorudi na bidhaa nyumbani na wanaoishia kuzitazama tu huko supermarket ni “kulipia bei”. Ukilipia bei, utarudi na bidhaa nyumbani.

Mungu akupe neema ya kushinda vita hii!

*“…Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.”* Ufunuo wa Yohana 2:11b

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**
Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Youtube: James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH Dodoma

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma   +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa
james_kalekwa
@MchungajiJK
+255 754 917 764